



## Reclaim Conservation

### Wenyeji na Wanaharakati Dhidi ya Dhulma za Mashirika za Uhifadhi

Tangu jadi, kumekuwa na miradi mengi yanayotekelezwa kote duniani kwa msingi wa uhifadhi wa mazingira. Haya miradi yanatumia jinsi nyingi tofauti ili kutimiza malengo yao ya uhifadhi wa mazingira, lakini hadi sasa, imedhihirika wazi kwamba hizi miradi hazijafanikiwa kufikia malengo yao. Licha ya ufadhili na uwekezaji wa kiwango cha juu mno, bado tunashuhudia athari za uharibifu wa maliasili, wenyeji kupoteza rasilimali zao, na hali ya mazingira kuendelea kuzorota.

Mashirika za kimataifa za uhifadhi hadi sasa wanaendelea kutegemea mashirika za kibiashara kwa ufadhili wa kazi zao kote duniani. Zaidi ya hao, kwenye miongo miwili hivi yaliyopita, wameanza kuiga mfano wa haya makampuni kwenye usimamizi na utendakazi wao katika nyanja za uhaifadhi wa mazingira na wanyama pori. Hali hii imezuia mashirika ya uhifadhi wasiweze kutimiza jukumu lao kwa sababu wengi wao wangejipata wanapinga au wanajaribu kurekebisha uharibifu wa mazingira unaotokana na utendakazi duni au sera duni za wafadhili wao.

Hatimaye wale tunaowategemea kutekeleza jukumu la kulinda au kuhifadhi mazingira yetu na rasilimali zetu hawawezi kamwe kuilfikia hili lengo. Kisa la maana ni kwamba hay mashirika ya uhifadhi wameingia kwenye orodha ya wale wanaofaidika kwa uharibifu au usimamizi mbaya ya mazingira kote duniani. Hawaungi tena mikono vyombo husika vya serikali, kwa sababu kuzorota kwa hivi vyombo iawafanya kunawiri zaidi na kupokea ufadhili maradufu. Wale tuliowategemea kutulindia rasilimali zetu basi wamekuwa washiriki katika uvujaji na uharibifu wa hizo rasilimali. Hali hii imekuwa chazo ya wao kututafutia suluhu zisizofaa, suluhu zisizokuwa na misingi yote za kijamii, na suluhu zisizoweza kudumu.

Licha ya hayo haya mashirika yamejitahidi kufunika uzembe wao kwa kuwalaumu wenyeji, wanavijiji, na wananchi wa kawaida kwa kila kisa cha uharibifu au ukiukaji wa sharia za uhifadhi wa mazingira. Usimamizi wa mali za kiasili umebadilishwa kuwa biashara ya fedha, na kila uchao, wenyeji hushawishiwa kuachilia haki zao za kutumia rasilimali zao ili wapewe rushwa fulani ya kifedha. Matokeo ya haya maovu yamekuwa ni ukiukaji wa haki za jamii, watu kuhamishwa makwao kwa nguvu, wafugaji kukosa malisho, na wenyeji kote duniani kupachikwa jina 'wahalifu' katika maswala yanayohusu uhifadhi wa mazingira. Mashirika ya uhifadhi wameedelea kujidai kwamba wao ndio 'walinzi halisi' wa mazingira na kwamba wanaharakati na wanavijiji ni uharibifu tu, wanaohujumu kazi ya uhifadhi wa mazingira. Kwa hivyo wanaendelea kuzuilia msaada isiweifike wadogo kutoka kwa wafadhili, wala hawataki kamwe kujaribu mbinu zozote mpya za usimamizi wa mazingira yanayo wajumuisha jamii.

Lengo letu kama 'Reclaim Conservation' ni kujikwamua kwenye hili mtaro na kuleta mabadiliko tukishirikiana na jamii, wasomi, vyuo vikuu, vyombo vya habari, na mashirika za serikali kubainisha wazi kwamba;

- **Uhifadhi ni Harakati**
- **Lazima tukomeshe ufasidi katika uhifadhi**
- **Hatutakubali ubaguzi wa aina yoyote katika uhifadhi**

**Bila huu msimamo, hatutafaulu!**